# Jorafra Transport Agency Ltd

*"Moving Business, Delivering Confidence"*

S.L.P 735, Mwanza, Tanzania | Jengo la Utawala Stand Kuu ya Mabasi Nyamhongolo, Ghorofa ya 1, Chumba Na. 59, Ilemela - Mwanza

**Simu / Phone:** +255 789 537 307 / +255 738 499 978 | **Email:** vacancy@jorafra.co.tz | **Website:** jorafra.co.tz

---

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI (SWAHILI)

Kampuni ya **Jorafra Transport Agency Ltd** inatangaza nafasi za kazi na inakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi mbalimbali za kazi katika matawi yetu kama ifuatavyo:

### NAFASI ZA KAZI NA SIFA ZAKE

---

| Nafasi ya Kazi | Idadi | Kituo cha Kazi | Sifa za Mwombaji |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Dar es Salaam Branch Manager** | Nafasi 1 | Dar es Salaam | • Shahada (Degree) au Stashahada ya Juu ya Usimamizi wa Biashara, Logistics, au fani inayofanana.<br>• Uzoefu wa kazi usiopungua miaka 2–3 katika nafasi ya uongozi/usimamizi. |

| Nafasi ya Kazi | Idadi | Kituo cha Kazi | Sifa za Mwombaji |
|---|---|---|---|
| | | | • Uwezo mkubwa wa uongozi, mawasiliano, na usimamizi wa rasilimali watu na shughuli za tawi. |
| **IT Specialist** Special Task | Nafasi 3 | Dar es Salaam / HQ | • Mkataba wa Mwaka Mmoja (1 Year Contract).<br>• Shahada (Degree) au Stashahada (Diploma) ya Sayansi ya Kompyuta, IT, au Software Engineering.<br>• Uwezo wa hali ya juu katika kusimamia mifumo, networks, na utatuzi wa changamoto za kiteknolojia. |
| **Sales Person** | Nafasi 3 | Dar es Salaam Branch | • Stashahada (Diploma) ya Biashara, Masoko (Marketing), au fani inayohusiana.<br>• **AU:** Kwa mwombaji asiye na Diploma, awe na **uzoefu wa kazi usiopungua miaka miwili (2)** katika mauzo na masoko.<br>• Uwezo mzuri wa kushawishi, kutafuta wateja wapya, na kujenga uhusiano mwema na wateja. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Sales Person** | Nafasi 2 | Mwanza HQ | • Stashahada (Diploma) ya Biashara, Masoko, au fani inayohusiana.<br>• **AU:** Kwa mwombaji asiye na Diploma, awe na **uzoefu wa kazi usiopungua miaka miwili (2)** katika mauzo.<br>• Awe mchangamfu, mwenye nidhamu ya kazi, na anayejua vyema soko la Mwanza na kanda ya ziwa. |

| Nafasi ya Kazi | Idadi | Kituo cha Kazi | Sifa za Mwombaji |
|---|---|---|---|
| **Logistics Officer**<br>**Mwanaume** | Nafasi 1 | Makao Makuu / Tawi | • Stashahada (Diploma) ya Procurement & Supply Chain Management, Transport Logistics, au inayohusiana.<br>• **AU:** Kwa mwombaji asiye na Diploma, awe na **uzoefu wa kazi usiopungua miaka miwili (2)** katika uratibu wa usafirishaji na ufuatiliaji wa mizigo.<br>• Uwezo wa kufanya kazi kwa umakini na chini ya msukumo (pressure). |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Office Assistant** | Nafasi 1 | Mwanza HQ | **1. Elimu na Uzoefu:**<br>• **Elimu:** Diploma au Cheti (Certificate) cha Secretarial Studies, Office Management, Business Administration, au fani inayohusiana.<br>• **Uzoefu:** Uzoefu uliothibitishwa usiopungua **miaka 1–2** katika majukumu ya usaidizi wa ofisi au sekretarieti.<br>**2. Ujuzi wa Kitendo na Taaluma:**<br>• **Ujuzi wa Kompyuta:** Umakini na uwezo mkubwa wa kutumia Microsoft Office (Word, Excel, PowerPoint) na usimamizi wa barua pepe/kalenda.<br>• **Uchapaji (Typing):** Kasi na usahihi wa kuchapa pamoja na umakini wa hali ya juu.<br>• **Utunzaji wa Kumbukumbu:** Ufahamu wa mifumo sahihi ya utunzaji wa nyaraka, mafaili na udhibiti wa nyaraka. |
| **Nafasi ya Kazi** | **Idadi** | **Kituo cha Kazi** | **Sifa za Mwombaji** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | • **Ujuzi wa Lugha:** Uwezo mzuri wa kuzungumza na kuandika kwa lugha ya **Kiswahili na Kiingereza** .<br>**3. Tabia na Ujuzi wa Kijamii (Soft Skills):**<br>• **Ujuzi wa Mawasiliano:** Mawasiliano mazuri na lugha ya staha, ukarimu na mtazamo wa kitaalamu.<br>• **Usimamizi wa Muda:** Uwezo wa kuweka vipaumbele, kupanga ratiba za mikutano/miadi, na kufanya majukumu mengi kwa wakati mmoja (multitasking).<br>• **Ushiri na Usiri:** Mwaminifu wa hali ya juu na mwenye kuzuia uvujaji wa siri za kiofisi na biashara.<br>• **Weledi:** Muonekano nadhifu, nidhamu ya kazi, na uwezo wa kujitegemea kufanya kazi bila usimamizi wa karibu. |

MAELEKEZO YA JUMLA YA ELIMU NA UZOEFU

- **Kiwango cha Elimu:** Kiwango cha chini ni Diploma kwa nafasi zote, *isipokuwa* kwa waombaji wa nafasi za Mauzo (Sales) na Logistics ambao hawana Diploma lakini wana uzoefu wa kazi usiopungua miaka 2.
- **Nafasi Zilizovuliwa Msamaha:** Nafasi za **Branch Manager** na **IT Specialist** zinahitaji elimu rasmi ya taaluma (Degree/Diploma) kama ilivyoelekezwa.

JINSI YA KUOMBA NA MASHARTI

Waombaji wote wanatakiwa kutuma **Barua ya Maombi ya Kazi iliyoandikwa kwa mkono** (Handwritten Application Letter) ikielekezwa kwa Uongozi wa Jorafra Transport Agency Ltd.

1. Viambatanisho vinavyotakiwa: **Curriculum Vitae (CV) mpya** na vyeti vya taaluma/uzoefu.

---

2. Dokumenti zote (Barua ya mkono, CV, na Vyeti) **ZIUNGANISHWE NA KUTUMWA KAMA PDF MOJA TU** .
3. Maombi yote yatumwe kwa barua pepe (Email): **vacancy@jorafra.co.tz**

## TAREHE MUHIMU ZA MAOMBI

---

### Muda wa Maombi: Maombi yanaanza kupokelewa kuanzia tarehe 03 Agosti 2026 hadi tarehe 10 Agosti 2026.

** Angalizo: Maombi yatakayowasilishwa kabla au baada ya tarehe zilizotajwa hayatachukuliwa hatua. Wanaostahili pekee ndio watakaopigiwa simu kwa ajili ya usaili.*